JINSI YA KUWA NA HEKIMA MBELE ZA MUNGU

Basi hekima yatoka wapi? na mahali pa ufahamu ni wapi? Akamwambia mwanadamu, Tazama, kumcha Bwana, ndiyo hekima; na kujitenga na uovu ni ufahamu. AYUBU 28:20, 28

Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima, wana ufahamu mwema wote watendao amri zake; sifa zake ni za milele. ZABURI 111:10

Ndipo nikaona ya kuwa hekima hupita upumbavu, kadiri nuru ipitavyo giza. MHUBIRI 2:13

Hekima humtia nguvu mwenye hekima kuliko mashujaa kumi waliomo mjini. MHUBIRI 7:19

Mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. Lakini na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote. Maana mwenye kusitasita ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo na kupeperushwa huku na huku. Kwa maana mtu huyo asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia mbili husitasita katika njia zake zote. YAKOBO 1:5-8

Ni nani miongoni mwenu aliye na hekima na maarifa? na aonyeshe kwa mwenendo mzuri matendo yake kwa upole wa hekima. Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, iliyosikika, imejaa rehema na matunda mema, haina ubaguzi, haina unafiki. YAKOBO 3:13, 17

Kumcha Bwana ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu. MITHALI 1:7

Heri mtu yule aonaye hekima, na mtu yule apataye ufahamu. MITHALI 3:13

Mwanangu, kama ukiyakubali maneno yangu, na kuyaficha maagizo yangu kwako; Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, na kuelekeza moyo wako upate kufahamu; Naam, ukiita maarifa, na kupaza sauti yako upate ufahamu; Ukiutafuta kama fedha, na kuutafuta kama hazina iliyositirika; Ndipo utakapofahamu kumcha Bwana, na kupata kumjua Mungu. Kwa kuwa Bwana huwapa watu hekima; kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu. Huwawekea wenye haki akiba ya hekima kamili; Huzishika njia za hukumu, na kuzilinda njia za watakatifu wake. Ndipo utafahamu haki, na hukumu, na adili; naam, kila njia njema. MITHALI 2:1-9

Pata hekima, jipatie ufahamu; usisahau; wala usiache maneno ya kinywa changu. Usimwache, naye atakuhifadhi; mpende, naye atakulinda. Hekima ni jambo kuu; basi jipatie hekima; na kwa mapato yako yote jipatie ufahamu. Mtukuze, naye atakukweza; atakuletea heshima, ukimkumbatia. Atakupa kichwa chako pambo la neema, Atakupa taji ya utukufu. MITHALI 4:5-9

Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima, na kumjua mtakatifu ni ufahamu. MITHALI 9:10

Kutenda maovu ni kama mchezo kwa mpumbavu; Bali mwenye busara ana hekima. Kinywa cha mwenye haki hutoa hekima, bali ulimi wa ukaidi utakatiliwa mbali. MITHALI 10:23, 31

Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu, bali hekima hukaa wanyenyekevu. Asiye na hekima humdharau jirani yake, bali mtu mwenye ufahamu hunyamaza.
METHALI 11:2, 12

Mtu atasifiwa kwa kadiri ya hekima yake, bali mwenye moyo wa ukaidi atadharauliwa. MITHALI 12:8

Kwa kiburi huja kushindana tu; Bali hekima hukaa nao wanaoshauriwa. MITHALI 13:10

Upumbavu ni furaha kwake aliyepungukiwa na hekima; Kumcha Bwana ni maonyo ya hekima; na kabla ya heshima ni unyenyekevu. MITHALI 15:21, 33

Si afadhali kupata hekima kuliko dhahabu! na kupata ufahamu ni kuchaguliwa kuliko fedha! MITHALI 16:16

Apataye hekima huipenda nafsi yake; Ashikaye ufahamu atapata mema. MITHALI 19:8

Inunue kweli, wala usiiuze; pia hekima, na mafundisho, na ufahamu. MITHALI 23:23

Apendaye hekima humfurahisha baba yake;
MITHALI 29:3

Fimbo na maonyo hutia hekima, bali mtoto aliyeachiliwa humwaibisha mamaye. MITHALI 29:15